

Learning by Ear 2009
Children's rights 02
Child labor

Topic: Child labor

Author: Mahamadou Koné (Mali)

Editor: Yann Durand

Translator: Anne Thomas

Kisuaheli Eric Ponda

	Women	Men	Age	
IN/OUTRO		X	Unimportant	
Narrator	X		Ca. 25	
Abdoulaye		X	16	
Moulaye Hassan Tall		X	Ca. 40	
Madani Doumbia		X	Ca. 30	

LbE Soundtrack

Intro

Hujambo mpenzi msikilizaji mahali popote ulipo na karibu kwa makala ya pili ya mfululizo wa vipindi vya “Noa Bongo Jenga Maisha yako” tukizungumzia masuala ya haki za Watoto na juhudi za kudumisha amani.

Mashirika mengi ya kimataifa na yale yanayotetea haki za binadamu yanapinga ukiukwaji wa haki za watoto na hasa ajira ya watoto hao. Mataifa mengi pia yameratibu na kutia saina maazimio haya kupiga marufuku ajira ya watoto. Lakini unyanyaswaji wa watoto bado unaendelea licha ya juhudi hizo. Hivi leo tunasafiri hadi Mali ambako Watoto wawili kati ya watano hufanya kazi. Tunakutana na Mtoto mmoja mwenye umri wa miaka 16 ambaye analazimika kufanya kazi baada ya kutoka Shuleni..

Report

1. Atmo Workshop: (sound of wood-cutting machine – at the end the boss says in Bambara "We are in the carpentry workshop": 24”

Narrator:

Karakana ya Madani Doumbia ni moja wapo ya karakana kubwa zaidi mjini Bamako, mji mkuu nchini Mali. Karakana hii ilianzishwa na Babake Madani mnamo mwaka wa 1949. Hapa kuna jumla ya wafanyi kazi 20, na 8 kati yao ni watoto wenye umri wa kati ya miaka 10 na 16.

Abdoulaye ni mfanyikazi katika karakana akiwa na umri wa miaka 16.

Amekuwa akifanya kazi mahala hapa kwa muda wa kati ya miaka 7 na 8 lakini hajakosa kwenda shule hata siku moja.

2. OTON : Abdoulaye (bambara): 26”

“Mimi bado ni mwanafunzi. Huamka saa 11 alfajiri kuoga kabla ya kupata kiamusha kinywa . Saa moja asubuhi naelekea shuleni. Na baada ya shule, mimi huja katika karakana hii kufanya kazi za

mkono. Na kisha baadaye kuelekea nyumbani mwendo wa saa 11 jioni. Nifikapo nyumbani kwanza huoga na kisha kuanza kutazama televisheni. Huwa silali kabla ya kufanya kazi zangu za shuleni.”

Narrator:

Na kama ilivyo kwa Abdoulaye, watoto wengi nchini Mali huishia kufanya kazi za mkono ambazo kwa kawaida zinapaswa kufanywa na watu wazima. Moulaye Hassan Tall ni meneja wa mpango wa taifa dhidi ya ajira ya watoto nchini Mali. Suala linalopewa kipaumbele na shirika la kimataifa la wafanyikazi nchini Mali.:

3. OTON: Moulaye Hassan Tall (French) : 28”

“Ni kweli, ni jambo la kuhuzunisha kwamba watoto wanalazimika kufanya kazi nchini Mali, na hali hii inazidi kuongezeka. Ripoti ya uchunguzi wa mwaka wa 2006 inaonyesha kuwa watoto wawili kati ya watano hufanya kazi nchini Mali, na mara nyingi ni kazi za hatari sana. Kazi ambazo zinaweza kudhuru afya yao, uthabiti, hali yao ya kisaikolojia na uwezo wa kukua vyema .”

Narrator:

Watoto wanafanya kazi kila mahali katika sehemu za miji na hata mashambani. Vijana kwa wasichana walio chini ya umri wa miaka 14 wanalazimika kufanya kazi. Baadhi yao kama Abdoulaye, hawafikiri kwamba wao ni wafanyikazi, bali watu wanaojifunza kazi na biashara. Lakini hali hiyo haibadilishi ukweli wa mambo, anasema Moulaye Hassan Tall:

4. OTON: Moulaye Hassan Tall (French) Length : 31''

“Utaratibu wa kufanya kazi uko wazi kabisa. Hakuna mototo aliye chini ya umri wa miaka 14 anapaswa kufayanya kazi nchini Mali, au hata kuwa mwanagenzi, isipokuwa tu anapopata kibali kutoka kwa idara ya Wafanyi kazi nchini. Tumetia saina maazimio yote mawili ya shirika la kimataifa la kazi, ILO. Azimio nambari 138 ambalo linauhusu tu kuanzia Mtu wa miaka 15 kuajiriwa, na pia azimio nambari 182 linalohimiza kupigwa marufuku aina yote ya ajira ya watoto na ukiukaji wa haki zao kufikia mwaka wa 2016”

5. Atmo Workshop (sound of polishing machine...) Length: 41''

Narrator:

Hata hivyo katika karakana hii anamofanya kazi Abdoulaye, watoto hawa hawateswi. Wao hufanya kazi kulingana na umri na nguvu zao. Meneja wa karakana hiyo Madani

6. OTON: Madani Doumbia (bambara): 20''

"Hapa watoto hawafanyi kazi ngumu. Hatuwaruhusu kutumia mashini zinazoweza kuhatarisha maisha yao au kuwajeruhi. Ni kweli wengine hutaka sana kutumia mashini kubwa lakini tunawashauri wachukue muda wa kujifunza kwanza- na pia kulinda afya zao".

Narrator:

Wazazi wengi wanatabia ya kuwaleta watoto wao kufanya kazi hapa. Huwa wanataka waanze kujifunza kazi mapema wakiwa wanga

wadogo. Lakini ni kinyume kabisa, kwani watetezi wa haki za Watoto wanasema kuwepo kwa watoto katika sehemu hizi ni hatari. Huyu hapa tena Moulaye Hassan Tall :

7.OTON : Moulaye Hassan Tall (French): 20”

“Hata kama watoto hawa wanaletwa na wazazi wao, hapa kuna vifaa vya hatari kama vile Patasi, Nyundo na misumari, na hawana vitu vya kujikinga kama vile viatu, glovu au hata miwani ya kujikinga na miale ya umeme wakati wazazi wao wanapochomelea vyuma. Na shughuli hizi zinaweza kuathiri afya zao..”

Narrator:

Abdoulaye ana bahati . Amekuwa akifanya kazi hiyo kwa muda wa miaka 10 na hajadhurika kiafya. Sio tu anapata ujuzi bali pia hurudi nyumbani na bakshishi mifukoni mwake. Anafurahia hali hii.

8. OTON: Abdoulaye (Bambara): 16”

“Napata riziki yangu kidogo hapa. Mimi hutengeneza bidhaa na kisha kuziua. Baadhi ya wakaazi hapa hunipa kandarasi ya kuwatengenezea vigoda, viti na fanicha nyenginezo. Nashukuru, napata riziki yangu.”

9. Atmo Workshop (Abdoulaye is assembling a photo frame) : 44

Narrator:

Raia wengi wa Mali hujifunza mapema kazi ya useremala au ufundi wa kuchomelea vyuma viwandani kwa sababu hujiunga na karakana hizi

wakiwa wadogo sana. Baadhi yao hujiunga na karakana hizi kwa sababu wanatafuta pesa kusaidia familia zao, na wengine kutaka kudadisi tu au kwa mapenzi yao wenyewe. Mwishowe huishia kufanya kazi hizi maishani. Madani Doumbia:

10. OTON : Madani Doumbia (Bambara): 39”

“Watoto wengi wanaokuja hapa huwa na azma ya kuwa wanabiashara siku za usoni. Na pindi wanapopata ujuzi, wengi huanzisha karakana zao. Baadhi yao huendelea kutafuta ushauri au hata msaada wa vifaa kama mashini kubwa kutoka kwetu. Watoto wengi wanaokuja hapa huwa wanataka kujifunza na sio kulipwa mshahara, lakini pia hutengeneza viti, meza na fanicha nyingine kwa kutumia mbao zinazosalia. Kisha huuza vifaa hivyo na kupata pesa kidogo za matumizi ..”

Narrator:

Abdoulaye anatoka familia yenye uwezo wa kadri. Hivyo hahitaji kuisaidia sana familia yake, lakini pesa zake hazikosi matumizi nyumbani, kama anavyosema.

11. O-Ton : Abdoulaye (Bambara): 17”

“Mimi natumia pesa zangu ninavyotaka. Huwezi kuwategemea wazazi kwa kila jambo. Mara nyingine hutumia pesa zangu kununua nguo na viatu au hata kwa starehe zangu mwenyewe”.

12. Atmo Workshop (employees are clearing the wooden planks away...) **Length : 19”**

Narrator:

Ajira kwa watoto ni hatari na ni kinyume cha sheria. Lakini je ni vipi mtu aliyekata tamaa maishani na hata kushindwa kutimiza mahitaji yake ya kimsingi anavyoweza kumkanya mtoto wake asifanye kazi? Suala hili bado ni changamoto kubwa hata kwa watetezi wa haki za binadamu. Na hapa tena ni Abdoulaye Hassan Tall:

13. Moulaye Hassan Tall (French): 20''

"Kama unavyojua nchi yetu ni maskini, kwa hivyo itakuwa vigumu kuwaambia wazazi tunataka kuwaondoa watoto hawa kutoka sehemu wanamofanyia kazi. Kwanza tunapaswa kuanzisha kampeni ya kuwaelimisha na kuwahamasisha watu kubadilisha tabia zao ili wazazi wafahamu kwamba mtoto wa umri wa kati ya miaka 12 na 14 anafaa kuwa shuleni."

14. Atmo Workshop (a young man is manually polishing wood with the help of a machine...): 1'19

Narrator:

Abdoulaye anafahamu fika umuhimu wa masomo yake lakini hata hivyo hawezi kupuuza kufanya kazi.

15. OTON - Abdoulaye (Bambara) Length : 10''

"Nawahimiza watoto wenzangu kwenda shule. Lakini wale wanaotoka familia maskini wanaweza kwenda shule na pia kufanya kazi katika karakana kama hii ili kujipatia riziki kidogo. Itakuwa kwa manufaa yao. "

Narrator:

Abdoulaye sasa ni mwanafunzi wa mwaka wa pili katika chuo cha taaluma mjini Bamako. Atakapomaliza atapewa cheti cha kufuzu katika masuala ya uhandisi na ujenzi. Yeye ameweza kumudu masomo na kazi. Na bila shaka ana matumaini makubwa maishani,

16. OTON Abdoulaye (Bambara) Length : 13”

"Azma yangu ni kumaliza masomo kwanza. Kisha badaye nitaangalia la kufanya. Aidha kutafuta kazi katika sekta ya umma au kuendelea na kazi mahali hapa au hata kuanzisha karakana yangu mwenyewe. Sioni tatizo lolote"

Narrator:

Labda Abdoulaye hana matatizo mengi yanayomuandama, lakini kuna maelfu ya watoto wenzake wanaondelea kunyanyaswa kwa kisingizio cha kujifunza kazi au kufunzwa kazi. Watetezi wa haki za binadamu wanasema kuwa watoto hawapaswi kuondolewa katika sehemu hizi za kazi na kisha kupelekwa katika vyojo kusomea kazi ngumu bila malipo.

End

OUTRO

Na hadi hapo ndipo tunapofika mwisho wa kipindi chetu kwa leo. Ripoti hii imeandikwa na Mahamadou Kone kutoka Mali. Unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao; tovuti yetu ni www.dw-world.de/lbe Ungana nasi tena wakati mwengine, Kwaheri!